102/1 MK
KISWAHILI
KARATASI YA 1
INSHA
MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA
MACHI 2022

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

KENYA CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION

KISWAHILI

KARATASI YA 1

# Mwongozo wa Kusahihishia

(SIRI)

MWONGOZO HUU WA KUSAHIHISHIA NI MILKI YA BARAZA LA MITIHANI YA KITAIFA LA KENYA (KNEC) NA SHARTI KUREJESHWA KWA BARAZA HILI BAADA YA USAHIHISHAJI

free revision content available at www.freekcsepastpapers.com

**Mwongozo huu wa kusahihishia una kurasa 5 zilizopigwa chapa.**

©2021 The Kenya National Examinations Council

1. Hii ni barua ya kirafiki.

Vipengele vifuatavyo vijitokeze:

**(a) Muundo**

Anwani ya mwandishi

Tarehe

**Kongowezi/Mtajo** – kwa mpendwa

**Utangulizi:** Maamkuzi yajitokeze

Uonyeshe anayeandika.

Unaweza pia kuonyesha kiini cha barua.

**Mwili** – hoja zijadiliwe hapa. Kila hoja kwenye aya.

**Hitimisho** –ajumuishe mawazo yake.

- Hitimisho kuhusiana na hoja/kiini cha barua ijitokeze

kimalizio- Jina la mwandishi.

**(b) Mtindo :** Mtindo wa barua ya kirafiki uzingatiwe. Mwandishi atumie lugha faafu inayozungumza moja kwa moja na anayeandikiwa.

**(c) Maudhui**

Mtahiniwa ajadili kikamilifu hatua ambazo kaunti imechukua kujitosheleza kwa chakula.

Baadhi ya hoja ni:

(i) Kaunti imehakikisha kwamba bei ya pembejeo za ukulima kama vile mbolea, mbegu na vifaa imepunguzwa ili kuboresha uzalishaji wa chakula.

(ii) Kuhifadhi maji ya mvua ili kunyunyizia mimea maji wakati ambapo hakuna mvua ya kutosha.

(iii)Kuimarisha/kuanzisha na kuhimiza utafiti kuhusu kilimo na ufugaji ili kuelekeza kuhusu njia bora za uzalishaji wa chakula

(iv)Kuwapa wakulima mikopo ili kuwawezesha kununulia pembejeo zinazohitajika.

(v) Kuimarisha miundomsingi,hasa barabara, mashinani ili kuimarisha usafirishaji wa chakula.

(vi)Kupanua soko ili kuwapa wakulima motisha kuzalisha chakula zaidi.

(vii) Kuboresha usimamizi na matumizi ya maji, hasa ya unyunyiziaji mashamba.

(viii) Kushirikisha sekta ya kibinafsi kuwekeza katika sekta ya kilimo.

(ix)Kuimarisha njia za uhifadhi wa mazao ili kukinga dhidi ya kuharibika/ ili yatumike kwa chakula wakati wa uhitaji.

(x) Kuwapa wakulima wa eneo kame mbegu zinazostahimili mazingira ya ukame ili itokeapo kwamba mvua itaacha kunyesha mapema, mazao yasiharibike.

(xi)Kuimarisha njia za kununua mazao ya ukulima na kuyahifadhi kwa matumizi wakati wa uhaba.

free revision content available at www.freekcsepastpapers.com

(xii) Kununua mifugo kutoka kwa wakulima wakati wa ukame na kutumia kupata nyama.

(xiii) Kuhimiza kilimo cha kisasa.

(xiv) Kuinyunyizia mimea dawa ili kukinga dhidi ya wadudu waharibifu.

(xv) Mikakati ya kuhakikisha kuwa fedha zilizotengewa uzalishaji wa chakula zinatumiwa kwa madhumuni hayo.

(xvi) Kutafuta njia mbadala ya kuzalisha chakula kama vile kufuga kuku wa kututumuliwa au kukuza mimea kama vile nyanya zinazokua kwa muda mfupi.

(xvii) Kuchimba visima au mabwawa ili kuhifadhi maji kwa matumizi ya baadaye.

(xviii) Kutojenga kwenye ardhi iliyotengewa upanzi wa mimea itoayo chakula.

(xix) Kuepuka shughuli zinazochangia mmomonyoko wa udongo, kama vile kulima kando kando ya mto.

**Tanbihi**

a) Pamoja na kwamba hii ni barua, inatoa taarifa/ habari kuhusu suala la kujitosheleza kwa chakula. Mtahiniwa sharti azingatie ukweli katika masuala anayojadili.

b) Vigezo vingine vya usahihishaji vizingatiwe kulingana na mwongozo wa kudumu.

c) Mtahiniwa atathminiwe kimaudhui kulingana na jinsi anavyojieleza.

d) Jina la kaunti linastahili kujitokeza. Hata hivyo, lisipojitokeza mtahiniwa asiadhibiwe. Atakuwa tayari amejiadhibu kimtindo.

2. Hii ni insha ya kutoa habari/arifu. Mtahiniwa anastahili kuandika insha ambayo inazingatia ukweli kuhusu manufaa/ haja ya kuimarisha miundomsingi. Anaweza kutoa mifano ya nchi ambayo iliimarisha miundomsingi na kupata manufaa.

Baadhi ya hoja ni:

(i) Kuboreshwa kwa barabara kumechangia usafiri wa haraka wa abiria na pia usafirishaji wa bidhaa. Umeokoa saa. Raia wametumia saa hizi kuzalisha mali.

(ii) Kukarabatiwa kwa mabomba ya maji kumepunguza mafuriko nyakati za mvua.

(iii) Upanuzi wa nyanja za ndege umechangia ongezeko la idadi ya wasafiri na hivyo kuboresha uchumi.

(iv) Kusambazwa kwa umeme katika sehemu za mashinani kumeinua hali ya maisha ya raia.

(v) Mifumo bora ya kutuma na kupokea pesa imerahisisha shughuli za ubadilishanaji wa bidhaa na huduma, na kuimarisha uchumi.

(vi) Kuboreshwa kwa barabara mashinani kumewezesha kupungua kwa gharama ya biashara na hiyvo kupungua kwa bei ya bidhaa muhimu. Hali ya maisha ya raia imeimarika kutokana na haya.

(vii) Kuboreshwa kwa mifumo ya usafiri kumechangia umoja na ushirikiano; raia wameweza kutangamana kwa wepesi.

(viii) Kuboreshwa kwa miundomsingi, kama vile mifumo ya mawasiliano kumechangia kuimarika kwa usalama wa kitaifa na kubadilishana mawazo kwa urahisi.

free revision content available at www.freekcsepastpapers.com

- Mtahiniwa aligetaja lakini mifano na kueleza manufaa yake
- Mwingine hatatambua miundomsingi lakini ameeleza manufaa ya miundomsingi.
- Mwingine hajui ~~kamuhimu~~ wa miundomsingi lakini ametajataja kila kwanza amejibu swali vizuri, wa pili hajajibu kikamilifu wa tatu wazi yake ikadiriwe; amepungukiwa kimaudhui. (Asipewe alama za hoja)
- Mtahiniwa atakayeeleza manufaa kisha ajadili hasara amejibu swali, usitoe maana za hasara.

(ix) Upanuzi wa hospitali na kuajiriwa kwa madaktari k kumeboresha huduma za matibabu na kuimarisha afya ya kijamii.

(x) Ujenzi wa shule na vyuo umeimarisha sekta ya elimu. Idadi ya watoto wanaojiunga na shule imeongezeka na kupunguza ujinga/ kupunguza asilimia ya watu ambao hawajui kusoma na kuandika.

**Tanbihi**

1. Dhana ya miundomsingi ni pana. Isichukuliwe tu ni barabara. Kuna miundomsingi ya kijamii kama vile shule na hospitali.
2. Mtahiniwa anaweza kuzingatia aina moja ya miundomsingi kama vile barabara, akatoa manufaa ya kuziimarisha.
3. Kigezo cha maudhui kikadiriwe kulingana na jinsi mwanafunzi anavyofafanua hoja. Hoja zifafanuliwe kikamilifu. Mwongozo wa kudumu urejelewe.
4. Kipengele cha muundo kitathminiwe kwa kuzingatia sehemu zifuatazo:
   (a) Utangulizi
   (b) Mwili
   (c) Hitimisho
5. Mwongozo wa kudumu uzingatiwe kwa usahihishaji wa kutegemewa zaidi.

3. a) Hii ni insha ya methali. Mtahiniwa anastahili kutunga insha ya masimulizi inayodhihirisha maana na matumizi ya methali hii.
b) Mtahiniwa atunge kisa kinachodhihirisha kwamba mtu ambaye hujiepusha na mambo yenye hatari/ athari/yanayoleta aibu, huepuka hatari/aibu/changamoto zinazotokana na hali hiyo.

c) Hali zifuatazo zinaweza kujitokeza:
(i) Msimulizi awe rafiki wa kundi linaloendeleza utovu wa nidhamu shuleni. Kundi lipange njama za kufisidi shule. Moja kati ya njama hizo inaweza kuwa kuchoma shule au tendo lolote la kihalifu. Msimulizi aone hatari katika haya; akatae kujiunga na kundi hilo. Ajiepushe na madhara kama vile kufukuzwa shuleni/kukatiza masomo yake/ kufungwa jela.
(ii) Msimulizi agundue kwamba wenzake wanadanganya katika mtihani. Akatae kushiriki katika tendo hilo. Matokeo ya mtihani ya wenzao yafutiliwe mbali. Yeye asalimike.
(iii) Msimulizi aonywe dhidi ya kushiriki katika vitendo hasi vya marafiki. Akaidi/ akose kusikiliza onyo hili. Ajiingize katika tendo hilo. Aathirike vibaya.
(iv) Msimulizi/Mtahiniwa anaweza pia kusimulia kisa cha jamii au nchi ambayo ilikataa kushiriki katika shughuli za kiuchumi au za kijamii ambazo nchi nyingine katika kanda zilishiriki kwazo. Shughuli hizo zinaweza kuwa kuziwekea baadhi ya nchi vikwazo vya kiuchumi, uundaji wa zana hatari za kivita, kushiriki katika tamaduni kandamizi/

free revision content available at www.freekcsepastpapers.com

zilizopitwa na wakati au hata kutumia maliasili kwa njia isiyo endelevu. Nchi hiyo iepuke athari mbaya za shughuli ambayo nchi au jamii hizo nyingine ziliendeleza.

**Tanbihi**

a) Lazima pande zote mbili za methali zijitokeze.

b) Mtahiniwa aonyeshe mhusika aliyejitenga na jambo hatari, kisha akasalimika /akaepuka madhara.

c) Mtahiniwa aonyeshe mhusika aliyejiingiza katika tendo hatari na kuathirika vibaya.

d) Mwongozo wa kudumu urejelewe katika utuzaji.

4. a) Hii ni insha ya mdokezo wa kuanzia.

b) Ni insha ya masimulizi. Mtindo wa kimasimulizi utumiwe.

c) Mtahaniwa atunge kisa ambacho kinaoana na mwanzo.

d) Kisa kionyeshe athari za mchezo wa bahati nasibu.

e) Kinaweza pia kuonyeha hali ambayo imemkumba anayetazamwa na Kutu hadi akawa amevunjikiwa kiasi hiki.

f)Ruwaza zifuatazo zinaweza kujitokeza:

(i) Mhusika aanze kucheza mchezo wa bahati nasibu. Mwanzoni ashinde kiasi. Apate kidogokidogo mshawasha wa kuendelea. Ashinde donge kubwa/pesa nyingi. Awe mraibu wa mchezo huu. Atumie pesa nyingi katika mchezo fulani, apoteze. Kila kitu. Ndipo anajiinamia.

(ii) Mhusika tajiri awe na mali nyingi ajiingize katika uchezaji huu ili atajirike zaidi. Apoteze kila kitu.

**Tanbihi**

i) Kisa kinaweza kuanza kisha kiturudishe nyuma kusimulia matukio ya awali hadi mhusika kufikia hali hii.

ii) Mtahiniwa anaweza kuanza kwa maneno hayo kisha kukiendeleza kisa moja kwa moja.

iii) Kwa vyovyote vile hali/toni ya kukata tamaa/ kuharibikiwa sharti ijitokeze.

iv) Kisa kinaweza pia kuwa na hali/toni ya kuharibikiwa, kisha mhusika akasaidiwa kujirekerbisha, insha ikawa na mwisho mwema.

v) Mja aliyekuwa ameinamia meza apewe jina. Hata hvyo, mhusika huyu anaweza kurejelewa kwa jina hilohilo, 'mja aliyekuwa kainamia meza,' kuanzia mwanzo hadi mwisho wa insha, mradi imedhihirika wazi ni huyuhuyu mhusika anayerejelewa katika swali.

vi) Mwongozo wa kudumu urejelewe katika utuzaji.

free revision content available at www.freekcsepastpapers.com